# Tunaweza kuwa na mjadala pevu kuhusu China tafadhali?:Jarida la Thelasini na Mbili (2022)



Wang Bingxiu  wa Klabu ya Shuanglang Farmer Painting (Dali Bai Autonomous Prefecture, China), *Untitled*, 2018.

Marafiki wapendwa,

Salamu toka dawati la Tricontinental: Institute for Social Research.

Wakati kiongozi wa bunge la Marekani Nancy Pelosi alipoingia Taipei,watu ulimwengunj kote walizizuia pumzi zao.Ziara yake ilikuwa ni kitendo cha uchokozi. Mwezi Desemba 1978,serikali ya Marekani – kufuatia uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1971 –ulioitambua Jamhuri ya watu wa China,unauweka kando mkataba wake wa awali wa majukumu yake kwa Taiwan.

Licha ya haya,Rais wa Marekani Jimmy Carter alisaini Sheria ya Mahusiano na Taiwan ya mwaka 1979, sheria iliyoruhusu viongozi wa Marekani kuendeleza mahusiano na Taiwan,ikiwamo kupitia mauzo ya silaha.

Uamuzi huu ni wa kuuzingatia hususani kwa hoja kuwa Taiwan ilikuwa ikiongizwa kijeshi tangu mwaka 1949 hadi 1987,ikihitaji ugavi wa silaha mara kwa mara.

Safari ya Pelosi huko Taipei ilikuwa ni sehemu ya muendelezo wa uchokozi unaoendelea wa Marekani dhidi ya China.Kampeni hii inajumuisha mpango ulioitwa 'pivot to Asia' wa Rais wa zamani Barack Obama, 'vita ya biashara' ya Rais wa zamani Donald Trump, uundwaji wa jumuiya za kiulinzi kama zile za Quad na AUKUS na kuigeuza taratibu NATO kuwa nyenzo dhidi ya China.Agenda hii inaendelea katika uamuzi wa Rais Joe Biden kwamba China lazima idhaifishwe kwa kuwa ndio 'mshindani pekee mwenye uwezo kutumia kwa pamoja nguvu zake za kiuchumi, kidiplomasia, kijeshi na kiteknolojia na kuibua changamoto endelevu' kwa mfumo wa ulimwengu unaotawaliwa na Marekani.

China haikutumia nguvu zake za kijeshi kumzuia Pelosi na viongozi wengine wa bunge la Marekani kusafiri kwenda Taipei.Lakini walipoondoka, serikali ya China ilitangaza kuwa itasimamisha maeneo nane muhimu ya kiushirikiano baina yake na Marekani,ikiwamo kukatisha mashirikiano kijeshi na kuahirisha mashirikiano ya kiraia kwenye maeneo mbalimbali, kama vile suala la mabadiliko ya tabia ya nchi.Hayo ndo mafanikio ya ziara ya Pelosi:yaani kuongeza makabiliano na kupunguza mashirikiano.

Kimsingi,yeyote mwenye kuamini juu ya mashirikiano mapana zaidi na China anajengewa taswira chafu katika vyombo vya habari vya Magharibi pamoja na vyombo vya habari washirika wa Magharibi vya Ulimwengu wa Kusini kuwa ni 'wakala' wa China ama mpigia chapuo 'upotoshaji taarifa'.Nilijibu baadhi ya tuhuma hizi katika gazeti la *Sunday News* la *Afrika Kusini* tarehe 7 Agosti 2022. Baki ya jarida hili inazaa makala hayo.



Ghazi Ahmet (Ukanda unaojitawala wa Xinjiang huko China,wenye jamii ya watu wa Uyghur), *Muqam*, 1984.>

Aina mpya ya ukichaa inazama katika uelekeo wa siasa za ulimwengu,ukungu wenye sumu unaokaba ufikiri.Ukungu huu,umesafiri kwa kuelea katika bahari ya fikra kongwe za *uzungu-bora(white supremacy)* na *ubabe wa umagharibi(western superiority)*,inaweka kiwingu katika fikra zetu kuhusu utu. Maradhi ya jumla yanayofuata ni kushukiwa na chuki ya kina kuhusu China , sio tu ya uongozi wake wa sasa au hata mfumo wa siasa wawa kichina, lakini chuki dhidi ya nchi yote na ya ustaarabu wa China -chuki juu ya *chochote* tu chenye kuhusika na China.

Kichaa hili kimefanya kuwepo na mjadala uliopevuka kuhusu China kusiwezekane.Maneno na misemo kama 'katili' na ' mauaji ya 'kimbari' yanarushwa kila mahala bila kujali juu ya hoja kama ni ya hakika. China ni nchi yenye watu bilioni 1.4 ,staarabu ya kale liyoteseka,kama sehemu kubwa ya ulimwengu wa Kusini ilivyoteseka, karne ya dhalili ,hii toka kipindi cha Vita vya Mihadarati vilivyolazimishwa na Waingereza (vilivyoanza mwaka 1839) mpaka mapinduzi ya China 1949 ambapo Mao Ze Dong alitangaza kuwa 'sasa watu wa China wameinuka'. Tangu hapo, jamii ya China imekuwa ikipiga hatua katika kutumia utajiri-jamii wake kukabiliana na matatizo ya muda mrefu kama vile njaa, elimu,kupoteza tumaini, na mfumo dume. Kama ilivyo

kwa majaribio yoyote ya kijamii, kumejitokeza matatizo makubwa, lakini hayo yanapaswa kutarajiwa toka kwa kundi la watu linalotekeleza jambo fulani.Badala ya kuitizama China kwa mafanikia na mikanganyiko yake, ukichaa huu wa zama zetu unalenga kuidogosha China kuwa kikaragosi cha Mashariki -dola la kikatili lenye agenda ya mauaji ya kimbari inayokusudia kudhibiti ulimwengu.

Kichaa hiki kina mahala mahsusi kilipoanzia nchini Marekani,ambako tabaka tawala la watu wachache linatishwa na kupiga hatua kwa watu wa China katika sekta za teknolojia za roboti, mawasiliano,reli za mwendokasi wa juu,na teknolojia za kompyuta.Maendeleo haya yanatishia vilivyo manufaa yaliyofurahiwa na makampuni ya kimataifa ya magharibi kwa muda mrefu, ambao wamefaidika na ukoloni kwa karne nyingi na pia joho la sheria za mali-maarifa(intellectual property).Hofu ya ulegelege wao na kuzidi kuungana kwa maendeleo ya kiuchumi baina ya Ulaya na kanda ya Ulaya-Asia kumepelekea wamagharibu kuzindua vita za taarifa dhidi ya China.

Wimbi hili kubwa la kiaidiolojia/nadharia linaeleke kuuzidi uwezo wetu wa kuwa na mazungumzo makini yenye msawazo kuhusu China na nafasi yake ulimwenguni. Mataifa mengi ya magharibi yenye historia ndefu ya ukatili wa ukoloni katika Afrika, kwa mfano, hupiga kelele juu ya wanachokiita ukoloni wa China katika Africa pasi kutambua juu ya jana ama uwepo wa kijeshi wa Ufaransa na Marekani uliokita mizizi maeneo mbalimbali barani.

Mashitaka juu ya mauaji ya kimbari mara zote huwa kwa watu wa rangi-ima iwe Darfur ama Xinjiang – lakini kamwe sio kwa Marekani, ambayo vita yake haramu nchini Iraq ilipelekea mauaji ya takribani watu milioni.Mahakama ya jinai ya Kimataifa (ICJ), imetopea katika fikra za mrengo wa Ulaya, kushitaki viongozi wa Afrika mmoja baada ya mwingine kwa uhalifu dhidi ya binadamu lakini katu kutowashitaki viongozi wa Magharibi kwa vita za ukandamijazi zisiokoma.



Dedron (Ukanda unaojitawala wa Tibet, China), *Untitled*, 2013.

Ukungu wa aina hii ya ukoloni mamboleo. Hivi karibuni, katika gazeti la *Daily Maverick* na the *Mail & Guardian*, nilishutumiwa kwa kusambaza ‘propaganda ya China na Urusi’  na kuwa na ukaribu na dola la kichama la China. Nini ulikuwa msingi wa  madai haya?

Mosi, chembechembe za ujasusi wa Magharibi zinajaribu kuupa taswira ukosoaji wowote wa mashambulizi ya wamagharibi kwa China kuwa ni propaganda ama upotoshaji taarifa. Kwa mfano, ripoti yangu ya Desemba 2021 kutoka Uganda ilikosoa daili lisilo la kweli kwamba mkopo wa China kwa nchi Ile ulilenga uwanja wake wa ndege wa kimataifa wa pekee kama sehemu ya mradi ovu wamtego wa madeni – fikra ambayo imekuwa ikikosolewa mara kwa mara na wanazuoni mahiri wa Marekani. Kupitia mazungumzo na maofisa wa serikali ya Uganda na kauli kwa umma kutoka Waziri wa Fedha Matia Kasija, Nilpata kujua, hata hivyo mkataba haukueleweka vilivyo na Dola lakini  hakukuwa na suala la kuukamata uwanja wa kimataifa wa Entebbe. Licha ya kuwa taarifa nzima ya *Bloomberg* juu ya mkopo huu ilijengwa katika msingi wa uongo, hawakuona haya kuisaidia Washington. Hiyo ndio namna ya vita vya taarifa.

Pili, kuna dai kuhusu kinachotajwa kama mafungamano yangu kwa Chama Cha Kikomunisti Cha China linaloegemea katika hoja nyepesi kuwa ninakutana wanataaluma wa China na nina nafasi nisiyolipwa katika Taasisi ya Taaluma za Fedha ya Chongyang katika Chuo Kikuu Cha Renmin,kituo mashuhuri cha wanafikra kilichopo Beijing. Cha kushangaza, machapisho mengi ya Afrika Kusini ambayo yameibua madai haya kichefuchefu yanafadhiliwa Taasisi ya George Soros’ Open Society Foundations. Soros alichukua jina la taasisi yake toka katika kitabu cha Karl Popper, *The Open Society and Its Enemies* (1945),ambamo Popper aliibua dhana ya ‘ustahimilivu usio na ukomo’. Popper alichombeza  juu ya mjadala wa hali ya juu  na kwamba maoni tofauti lazima yajibiwe kwa ‘hoja makini’.Zipo wapi hoja makini hapa, katika kampeni chafu zinazosema kwamba kujadiliana na wanataaluma wa China linalopaswa kuwa na ukomo ila kujadiliana na maofisa wa Marekani ndo kwapaswa kukubalika? Ni ngazi ngani ya ukaburu wa staarabu inayozalishwa hapa, ambapo waliberali katika Afrika Kusini wanashadadia ‘makabiliano ya staarabu’ zaidi kushinda  ’mjadala baina ya staarabu’?

Mataifa katika ulimwengu wa kusini yanaweza kujifunza vilivyo kutoka katika majaribio kisoshalisti ya China.Kufuta kwake umasikini uliokithiri katika janga la kiulimwengu la gonjwa la mlipuko -mafanikio yanayosheherekewa na Umoja wa Mataifa -yanaweza kutufunza ya kukabili hoja inda zinazofanana katika mataifa yetu(Ndio sababábu Tricontinental: Institute for Social Research iliandaa utafiti wa kina juu ya mbinu zilizotumiwa na China kupata mafanikio haya makubwa).Hakuna nchi katika dunia iliyo timilifu,na hakuna iliyo juu ya ukosoaji.Lakini kuendeleza tabia ya kushuku dhidi ya nchi moja na kujaribu kuitenga ni hatari kijamii. Kuta zapaswa kuangushwa, si kujengwa.

Marekani inachochea mgogoro sababu ya hofu zake kwa China kutokana  na kupiga hatua kwa China kiuchumi: tusifanywe mazuzu wa maana. Tunahitaji mjadala uliopevuka kuhusu China, mijadala tunayolazimishiwa na maslahi makubwa ambayo si ya yetu.




Yang Guangqi wa klabu ya Shuanglang Farmer Painting(Dali Bai Autonomous Prefecture, China), *Untitled*, 2018.

Makala yangu katika *The Sunday Times* hayafafanui masuala yote yanayojiri katika suala la mgogoro' baina ya Marekani na China.

Hata hivyo,ni mualiko kwa mjadala.Kama una mawazo juu ya masuala haya, tafadhali nitumie barua pepe.

Kwa huba,

Vijay

Imetafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza na Muhemsi Mwakihwelo.